

**OFISI YA RAIS TAMISEMI  
HALMASHAURI YA WILAYA YA BUSOKELO**

**SIMU: 0756488177  
0655707527**

**SHULE YA SEKONDARI ISANGE,  
S. L. P 269,  
TUKUYU.**

**11/12/2020**

**YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI ISANGE KIDATO  
CHA KWANZA MWAKA 2021.**

Napenda kukujulisha kuwa umechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza katika shule hii. Hivyo unatakiwa kuripoti shuleni tarehe 11/01/2021 siku ya Jumatatu saa 1:00 asubuhi.

**MAHITAJI:**

**A. SARE ZA SHULE.**

- i) Wavulana wanatakiwa kushona suruali mbili (2) za heshima (khaki tetroni na nyeusi)
- ii) Wasichana wanatakiwa kushona sketi mbili (2) za heshima kuvuka magoti (rangi ni khaki tetroni na nyeusi)
- iii) Kila mwanafunzi awe na sweta lenye rangi ya kijani na jaket jeusi lisilo na maandishi yoyote.
- iv) Mashati mawili meupe tetroni mikono mifupi kwa wavulana na wasichana
- v) Viatu vya ngozi rangi nyeusi vyenye kamba visigino vifupi jozi mbili, wasichana wataruhusiwa kuvaa viatu aina ya bajaji wakati wa mvua tu.
- vi) Kila mwanafunzi anatakiwa kuvaa raba nyeusi siku ya Ijumaa (Siku ya michezo).
- vii) Kila mwanafunzi ajinunulie track suit rangi ya kijani itavaliwa siku ya Ijumaa.
- viii) Kila mwanafunzi awe na fulana ya dark blue yenye kola na nembo ya ya shule (10000/= ailete shuleni) ataivaa siku ya Alhamisi (Uamuzi wa kikao cha wazazi tarehe 9/6/2016)

**IKUMBUKWE:** Sare hizo zitakaguliwa siku ya kuripoti.

**VIFAA VYA DARASANI & USAFI.**

Kila mwanafunzi anatakiwa kuwa na:-

- i. Begi la kubebea madaftari.
- ii. Madaftari makubwa kumi (kuanzia Quire 3)
- iii. Mkebe mmoja, rula na kalamu za wino za kutosha.
- iv. Ndoo lita kumi moja, kwanja moja, jembe lenye mpini na ufagio wa chelewa mmoja (wenye thamani ya sh 2,000/=)

## **CHAKULA CHA MCHANA KWA WANAFUNZI**

Kila mwanafunzi alete:

- i. Mahindi debe mbili (2) kwa mwaka.
- ii. Maharage Kilo 2 (BP nne 4) kwa mwaka.
- iii. Tsh. 5,000/= kwa ajili ya kumlipa mpishi, kusagia mahindi na kununua chumvi (Hakikisha unapewa risiti ukilipa)- (Uamuzi wa kikao cha wazazi cha tarehe 14/03/2018)

## **MAAGIZO KWA WATAKAOKUWA HOSTEL (WASICHANA TU)**

- i. Ada ya hostel Tsh 550,000/= italipwa awamu tatu (Ya **kwanza (Januari 2021) =250,000/=, ya pili (Aprili 2021) =150,000/= nay a tatu (Agosti 2021) =150,000/=**).
- ii. Godoro futi mbili na nusu moja.
- iii. Shuka mbili (pink na bluu bahari)
- iv. Trunker moja
- v. Blanket moja
- vi. Sahani moja, kijiko kimoja na kikombe kimoja.
- vii. Sketi rinder box mbili za kijivu za kushindia (ndefu iguse unyayo wa mguu), nguo za nyumbani haziruhusiwi.

## **MAAGIZO MENGINE:**

Mwanafunzi anatakiwa kuleta

1. Chet cha kuzaliwa
2. Fomu ya daktari toka kituo kinachotambulika yenye majibu ya vipimo vyake vya afya.
3. Nakala ya sheria na kanuni za shule (atapata akifika shuleni)
4. Kuleta ream moja ya karatasi kwa mwaka, (karatasi kwa ajili ya mitihani)
5. Tsh 10,000/= kwa mwaka, kwa ajili ya posho ya mwalimu wa hesabu (shule ina upungufu wa waalimu wa hisabati, shule hulazimika kuajiri mwalimu wa muda)- (Uamuzi wa kikao cha wazazi cha tarehe 19/01/2017)
6. Tsh 5000/= ya bima ya afya kwa wasio na bima (Kama unayo utaionesha shuleni siku ya kuripoti)

Nakutakia utekelezaji mwema.

**JACOB J. MALASUSA**  
**MKUU WA SHULE**

## **Nakala:**

- a. Afisa elimu kata,  
Kata ya Isange,  
S. L. P 2,  
**TUKUYU.**
- b. Afisa elimu sekondari,  
Halmashauri ya wilaya ya Busokelo,  
S. L. P 2,  
**TUKUYU.**

## MEDICAL CERTIFICATE FORM

STUDENT NAME.....

To be completed by a Government Medical Officer or a doctor from a recognized health institution in respect of form one entrant. Please examine the above as to her/his physical and mental fitness as a student at this school.

The examination should have to involve the following categories

1. Vision with glasses right ..... left.....
2. Blood pressure .....
3. Hemoglobin .....
4. F. V. Bleeding .....
5. Urine for sugar. ....
6. Stool for routine examination .....
7. Venereal diseases .....
8. Neurosis .....
9. T. B. Test .....
10. Any abnormality
  - a) Heart .....
  - b) Lung .....
  - c) Spleen .....
  - d) Chest .....
11. Is there any serious disease e.g. Leprosy, Epilepsy, Asthma, Diabetes .....

Doctor's name.....

Signature and official stamp

.....

Date .....